**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**

**Simu:** Mkurugenzi: +255-28-2501375 S. L.
P 1333
**Ofisi zote: +**255-28-40334
**MWANZA**
**Nukushi:** +255-028-2500785
**Barua pepe:** cd@mwanzacc.go.tz
info@mwanzacc.go.tz
**www.mwanzacc.go.tz**

30, Aprili, 2018

# TANGAZO

## ZABUNI YA HUDUMA YA USAFI, UKUSANYAJI, USAFIRISHAJI WA TAKA NGUMU HADI DAMPO NA UKUSANYAJI WA ADA YA TAKA NGUMU KWA MWAKA 2018/2019

## ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02

Halmashauri ya Jiji la Mwanza inapenda kualika Kampuni zilizosajiliwa kisheria na mamlaka husika, zenye uwezo wa kifedha na vitendea kazi vya kisasa ili kuweza kutoa huduma bora ya Usafi, Ukusanyaji na Usafirishaji wa Taka ngumu kwa Wananchi, Taasisi na Wadau mbalimbali waliomo ndani ya Jiji pamoja na Ukusanyaji wa Ada ya Taka ngumu kutoka kwa wateja wanaopatiwa huduma hiyo. Maeneo yatakayopewa huduma yamebainishwa kwenye Jedwali na. 1.

**Jedwali 1:** Maeneo yaliyobainishwa kwa ajili ya huduma hiyo

| **Fungu Na.** | **Maelezo** [orodha ya kina, ya maelezo ya mahitaji ] | **FUNGU LA KUTOLEA ZABUNI** |
|---|---|---|
| 1. | KATA ZA PAMBA, MBUGANI NA IGOGO | ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02/1 |
| 2. | KATA ZA NYAMAGANA, ISAMILO NA MIRONGO | ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02/2 |
| 3. | KATA ZA MABATINI, MAHINA NA MHANDU | ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02/3 |
| 4. | KATA ZA BUTIMBA NA MKOLANI | ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02/4 |
| 5. | KATA ZA IGOMA NA KISHIRI | ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02/5 |
| 6. | KATA ZA NYEGEZI, MKUYUNI NA LUCHELELE | ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02/6 |
| 7. | KATA ZA BUHONGWA NA LWANHIMA | ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/02/7 |
| | | |

**Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-**

i) Ada ya maombi ya zabuni ni shilingi **laki moja tu (100,000/=) kwa kila fungu** ambazo hazitarejeshwa. Mzabuni atatakiwa kuambatanisha nakala halisi ya risiti ya ada ya maombi. Ada hii ni kwa maombi ya kila fungu kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali namba 1.

ii) Ada ya maombi itakayolipwa ni kwa ajili ya kupata maelekezo ya zabuni (Tender Document). Katika kabrasha la zabuni (Tender Document) kuna sifa, vigezo na masharti muhimu

yanayotakiwa kutimizwa na kila mwombaji wa zabuni. Aidha maelekezo zaidi kuhusiana na zabuni hii yanapatikana kwa Katibu wa Bodi ya zabuni.

iii) Kampuni itakayoomba zabuni iwe imesajiliwa kwa mujibu wa sheria na mamlaka husika ya BRELA. Nakala halisi ya **CHETI CHA USAJILI** (Company Registration Certificate) iambatanishwe na iwe imeidhinishwa (certified) na wakili anayetambulika kisheria.

iv) Kampuni itakayoomba iwe na usajili wa **CHETI CHA OSHA** (Occupational Safety and Health Authority certificate).

v) Kampuni itakayoomba iwe na ofisi zinazotambulika rasmi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anwani kamili ya mahali ofisi zilipo ionyeshwe kwenye maombi ya zabuni.

vi) Kampuni itakayoomba iambatanishe nakala ya miamala ya benki (Bank Statement) iliyothibitishwa na Benki husika kuanzia Januari, 2018 hadi kutolewa kwa tangazo hili.

vii) Kampuni itakayoomba zabuni iwe na uthibitisho wa ulipaji kodi za Serikali kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Nakala halisi ya usajili wa TIN (Tax Identification Number) iambatanishwe.

viii) Kampuni itakayoomba zabuni iwe na magari maalum yasiyopungua matatu (3) kwa ajili ya kusafirishia taka ngumu. Magari mawili (2) yawe aina ya Compactor trucks na Canter moja (1) yenye ujazo wa tani saba (7) itakayotumika kukusanya taka ngumu kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi. (Uonyeshe uhalali wa magari hayo au mikataba ya Ukodishaji)

ix) Kampuni itakayoomba zabuni iwe na uzoefu wa muda usiopungua miaka mitatu (3) katika shughuli ya Usafi, Ukusanyaji na

x) Usafirishaji wa Taka Ngumu kwenye mamlaka za Jiji na Manispaa zilizopo nchini Tanzania. (Uonyeshe uthibitisho wa uzoefu huo)

xi) Kampuni itakayo fanikiwa kupata zabuni hii itakusanya Ada ya taka ngumu kutoka kwa wateja kwa kutumia mfumo wa ki electronic POS wa Halmashauri ya Jiji.

xii) Kampuni itakayoomba zabuni iwe na wataalam wasiopungua wawili (2) wenye uzoefu wa kutosha na waliohitimu Shahada katika fani za Usimamizi wa Mazingira (Environmental Management), Afya ya Mazingira (Environmental Health), Uhandisi wa Mazingira (Environmental Engineering/Sanitary Engineering). Wataalam hao wasiwe watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Nakala halisi ya vyeti vya Shahada vya wataalam vilivyothibitishwa viambatanishwe ndani ya maombi ya zabuni.

xiii) Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iambatanishe orodha kamili ya viongozi pamoja na wasifu wao (Curriculum Vitae). Viongozi wawe ni wale watakaosimamia moja kwa moja utekelezaji wa zabuni hii.

xiv) Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iwe na vitendea kazi bora na vya kisasa kwa ajili ya kufagia, kukusanyia taka ngumu, kuwakinga watumishi na ajali/ madhara mbalimbali pamoja na vyombo vya kusafirishia taka ngumu kutoka kwenye maeneo ya kaya, biashara, stendi, masoko na maeneo ya wazi na kuzipeleka kwenye vituo vya kukusanyia taka ngumu (collection points) zilizoidhinishwa kutumika na Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

xv) Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iambatanishe wasifu wake (Organizational Profile) inayoonyesha uzoefu wa utoaji wa huduma ya Usafi , uzoaji na Usafirishaji wa taka ngumu kwenye mamlaka za Jiji na Manispaa mbalimbali zilizoko nchini.

xvi) Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iambatanishe **TAMKO RASMI DHIDI YA VITENDO VYA RUSHWA** iliyosainiwa na mwombaji mwenyewe.

xvii) Kampuni itakayochaguliwa kutekeleza zabuni hii itapaswa kuleta dhamana ya kufanya kazi kwa njia ya Banker's Cheque kutoka benki husika yenye thamani ya malipo ya miezi mitatu (3) ya kiasi alichoahidi kuilipa Halmashauri. Hii ni kwa wazabuni watakaoshinda zabuni hii.

xviii) Kampuni itakayoomba zabuni iwasilishe zabuni Halisi (Original) moja (1) na nakala( Copy) mbili (2), endapo maelezo ya original na nakala yatatofautiana Original ndio itatumika kwenye tathmini.

xix) Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yeyote (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya fungu la zabuni, kazi inayoombwa, “Original & Copy”, anuani kama ilivyoelekezwa bila kuwekwa alama yoyote.

xx) Kampuni inayoomba ikishindwa masharti yaliyotajwa kwenye tangazo hili itakuwa imejiondoa kwenye mchakato mzima wa zabuni.

xxi) Uongozi wa Halmashauri ya Jiji Mwanza haulazimiki kuchagua zabuni yoyote.

xxii) Barua zote za maombi ya zabuni zifungwe kwa LAKIRI na ziandikwe namba ya fungu la zabuni iliyoombwa na zipelekwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Ghorofa ya pili na kuwekwa katika sanduku la zabuni.

**Juu ya bahasha iandikwe fungu unaloomba:**
**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,**
**HALMASHAURI YA JIJI,**
**S.L.P 1333,**
**MWANZA.**

xxiii) Kampuni itakayoomba zabuni inaruhusiwa kuomba fungu zaidi ya moja (1) na yasiyozidi mawili (2) na kila sehemu ni lazima alipe ada ya maombi ya shilingi **laki moja tu (100,000/=)** ambazo hazitarudishwa.

xxiv) Mwisho wa kupokea zabuni ni saa nne (4) kamili asubuhi (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **15/05/2018, Siku ya Jumanne katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza.** Waombaji au wawakilishi wao wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi Mkubwa katika ofisi za Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

xxv) Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (E-mail) hazitashughulikiwa.

KIOMONI KIBURWA KIBAMBA
**MKURUGENZI WA JIJI**
**MWANZA**